# Zaburi 18

***Siku ya Mungu ya 3 ya kwarezima***
***Mwaka B***

***Gauthier KM***




1. Sheria ya Bwana ni kamilifu,
   yatuliza roho;
   mafundisho ya Bwana ni imara,
   yamletea mjinga elimu

2. Amri za Bwana ni zahaki,
   zafurahisha moyo;
   agizo la Bwana ni safi ,
   layatia macho mwangaza

3. Ibada kwa Bwana ni safi ,
   ya dumu hata milele;
   hukumu za Bwana ni kweli ,
   zote za haki kamili

4. Zatamanika kuliko zahabu,
   kuliko wingi wa zahabu safi ;
   ni tamu kuliko asali ,
   kuliko mavuno ya uki .